# METHALI KATIKA JAMII YA WANANDI: CHIMBUKO NA UAINISHAJI WAKE

Naomi, C. Jescah. na Biwott, K. Anthony
2018 TUKI; Dar es Salaam

## Ikisiri

*Makala haya yanaangazia chimbuko la "kalewenoik" yaani methali za Kinaandi na uainishaji wa methali zenyewe huku yakijaribu kubainisha hadhira iliyotungiwa methali hizo. Kwa mfano iwapo zilitungiwa watu maalum na iwapo zilisemwa wakati maalum. Aidha, tumeshughulikia malengo ya methali katika jamii ya Kinandi pamoja na umuhimu kwa wasemaji, wasemewa na jamii kwa jumla. Tumejaribu pia kutafsiri baadhi ya methali hizi na kutolea maana na matumizi katika jamii husika. Hii ni kutokana na utafiti uliofanyika katika Kaunti ya Nandi na Uasin Gishu ambapo tuliwasaili wazee 15 tofauti wenye umri wa miaka 65 na zaidi.*

**Maneno ya Msingi:** ***Methali, Chimbuko, Uainishaji***

## 1.0 Utangulizi

Fasihi ya Afrika na hasa fasihi simulizi haijaandikiwa sana vitabuni. Japo tafiti finyu zimefanywa, mengi hayajapata kunakiliwa vitabuni, ni machache tu ndiyo yaliyopata kupenyeza vitabuni. Maandishi ya mwanzoni yaliandikwa na wageni kama vile Ruth Finnegan katika kitabu chake cha *Oral Literature in Africa* (2012). Hata hivyo, tafiti ambazo zimeendelezwa na Waafrika zimechunguza fasihi simulizi kwa jumla kwa mfano, Mulokozi (1989), alichunguza tanzu za fasihi simulizi. Tafiti ambazo zimeangazia semi kwa mfano, zimeshughulikia maana, maudhui, dhima, muundo, lugha na matumizi (Lubaleje 1990, Momanyi 2006, Vifu 2006). Katika makala haya, tunapiga hatua zaidi kwa kuchunguza chimbuko la methali na uainishaji wake katika jamii ya Wanandi. Katika jamii ya Waafrika, maadili mengi bado yako kwenye mazungumzo, na mengi yanasahauliwa kwa sababu ya athari kutoka kwa tamaduni za kigeni ambazo zimeenezwa barani Afrika kwa wepesi kupitia kwa maendeleo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEKNOHAMA).

Semi ni mojawapo ya nyenzo muhimu katika maingiliano ya wanadamu katika maisha yao ya kila siku. Mazungumzo au maandishi yanayoambatanishwa na semi huwa na mvuto wa ajabu kwa msomaji sawa na msikilizaji. Misemo hufanya mawasiliano kuwa wazi zaidi na kamili. Kunazo semi nyingi iliyo na busara na hekima katika jamii ya Wanandi ambayo haijaandikwa vitabuni. Kwa hivyo, kuna haja ya kuandikia semi hizi ili watumiaji wote wanufaike na dafina hizi za lugha ya Kinandi. Iwapo semi hizi zitaandikwa, zitasaidia kufafanua utamaduni wetu ambao hivi sasa tunauhitaji mno. Methali ni mojawapo ya semi ambayo inaweza kuwa na matumizi ya namna nyingi hasa katika jamii ya Wanandi kulingana na mazingira yao.

Kwa mujibu wa Mulokozi (1989), methali ni semi fupi fupi zenye kueleza kwa muhtasari fikra au mafunzo mazito yanayotokana na uzoefu wa kijamii. Katika jamii ya Wanandi, mawazo haya huelezwa kwa kutumia sitiari na mafumbo. Hii inadhihirisha kwamba methali imesheheni usanii mkubwa, na kupitia kwayo utamaduni wa Wanandi unakuzwa. Madhumuni ya kuziandikia methali hizi ni kur ahisisha upatikanaji wake. Zaidi ya hayo, huu ni wakati mwafaka wa kuzijengea uhalali na hadhi yakinifu ya methali za kinandi ili kwenda sambamba na maendeleo endelevu ya kisayansi na teknolojia. Kwa hivyo, makala hii itaangazia chimbuko la methali katika jamii ya Wanandi na uainishaji wake.

## Wanandi

Jamii ya Wanandi ni pana, ni mojawapo ya jamii ya wanailotiki ambao wanazungumza lugha ya Kikalenjin ambayo ndanimo mna lahaja zifuatazo: Kisabaot, Kikipsigis, Kikeiyo, Kinandi, Kimarakwet, Kitugen, Kipokot na Kiterik. Jamii hii ina historia ndefu kuanzia nchi ya Israel, Misri, Sudan, Uganda hadi Kenya, hasa sehemu za magharibi mwa Bonde la ufa. Mtawanyiko wao unatokana na lahaja zao. Kwa mujibu wa sensa (2009) idadi ya Wanandi yapata milioni 4.9. Licha ya kufanya makao katika mkoa wa Bonde la ufa, na hasa katika kaunti za Nandi, Uasin Gishu na Transzoia, kuna wale wanaoishi chini ya milima ya Aberdare na kule Morogoro (*Morgor)* Tanzania. Jamii hii ni ya wafugaji hasa wa ng'ombe wa maziwa pamoja na ukulima wa mahindi, ngano na chai.

## Chimbuko la methali

Kuna mielekeo miwili mikuu kuhusu usuli wa methali katika jamii ya Wanandi. Ilivyo ni kwamba, methali zilitokana na ngano au hadithi zilizotambiwa watoto ili kutoa mafunzo fulani ya maisha. Aidha, kuna zile zinazotokana na hali au mazingira ya mwanadamu.

## Methali zilizotokana na Ngano

Ngano ni hadithi za kimapokeo zitumiazo wahusika kama wanyama, miti na watu kuelezea au kuonya kuhusu maisha. Ni utanzu ambao unajumuisha fani kadha, kama vile; istiara, mbazi, na hata kisa. (Mulokozi, 1989). Madai haya ya Mulokozi yanashabihiana na mwelekeo wa Wanandi kuhusu usuli wa methali. Baadhi ya methali zao zinatokana na visa mbalimbali ama vilivyotokea au vya kubuni. Visa hivi vilitambiwa watoto wadogo usiku kabla ya kulala. Mara nyingi vilitangulizwa na vitendawili ambavyo hadhira (watoto) walitegeana na kuteguliana. Hili lilifanywa kimakusudi ili kuteka hisia zao na makini pamoja na kutia makali kumbukumbu zao kabla ya kutambiwa hadithi na bibi au babu. Kwa hiyo ni mafunzo ya hadithi yaliyofumbwa na kutumika kutunga methali. Ujumbe unaojitokeza katika methali hizi huwa ni wa kutahadharisha, kuogofya, kuonya na hata kuelimisha. Uteuzi wa maneno na taswira zinazotumiwa hutoa picha ya ukanaji ambayo huashiria matokeo mabaya yatakayompata asiyetii amri.

Ni katika kiwango hiki ambapo uelewa wa mtu wa maana ya methali unategemea pakubwa yale mafunzo aliyoyapata kutokana na hadithi alizotambiwa utotoni. Kwa hivyo, fumbo lililoko

kwenye methali linalingana na lile fumbo kwenye hadithi. Nyingi ya methali za Kinandi zina msingi wa hadithi. Mfano;

a) *Ngo samis Muryaat kobo koot nebo* (Hata ikiwa panya yuavunda, ana kwao)

Methali hii ni zao la hadithi simulizi ya uhasama wa kaka wawili:

Katika zama zisizohesabika, paliishi kaka wawili wazawa wa tumbo moja, katika kijiji kimoja miongoni mwa jamii ya Wanandi. Ndugu hawa waliishi kwa utangamano aushini mwao kabla ya mauko ya wazee wao. Miaka ya mwanzoni mwa uyatima wao ilikuwa shwari hadi pale ambapo mmoja wao alihiari kufunga ndoa. Majilio ya mwanamke yakazaa matunda ya uhasama miongoni mwa kaka hao. Matunda haya yalipopevuka, mizozano ya kila mara ikaanza kushuhudiwa katika aila ile. Yule kaka aliyekuwa hajaoa akahiari kuguria nchi ya mbali na kuapa kutorudi tena hata kwa mtutu wa bunduki. Kwa vingine, ilikuwa njia moja ya kuepuka balaa.

Zilipita miaka mingi kabla ndugu hao kuonana. Tamaa ya yule kaka aliyebaki nyumbani ya kuonana na kakake ilizidi. Kwa hivyo, akaanza kufikiri afunge safari ya kumsaka kakake lakini wapi? Juhudi hizi zilikuwa kama za kutafuta sindano katika shamba la ngano. Hii ni kwa sababu hakuwa na habari zozote kuhusu alikoguria nduguye. Ilimbidi awaze zaidi, na mwisho mawazo yake yakapata mashiko. Aliamua kupanga njama, njama ya kumuua panya kisha kumtia kwenye *teret* (chungu) na kukiweka *tabut* (darini) na kujificha kuko huko darini.

Siku zilipita, mke wake kwa ushirikiano na jirani zao walimtafuta kila mahali wasimpate. Uvundo wa yule panya ukaanza kutoa mwelekeo. Yule mwanamke alipogundua kulikotokea harufu, alianza kupiga nduru akisema kuwa mumewe amejinyonga darini. Jirani zao kusikia habari zile za tanzia, kinyume na matarajio, waliamua kujitenga na kifo kile na hata kuhamia kwingine. Mkewe 'marehemu' naye akaamua kufunga virago vyake na kurudi kwao. Kama ilivyokuwa ada, mtu akifa jamaa zake wa damu ndio waliomzika. Ujumbe wa kifo ulipomfikia yule kaka, akaamua akarudi nyumbani. Alipofika nyumbani, alijitoma darini kwa shughuli za kuitoa ile maiti ya kakake kwa ajili ya mazishi. Kule darini, alishangaa kumpata kakake yu hai, wakapigana pambaja na kusameheana. Mwisho waliishi kwa utangamano. Hadithi hii inatufunza kwamba, ndugu yako hata awe mbaya kiasi gani, yafaa umpende na muishi kwa kusameheana kwa kuwa ndiye anayekujali katika kila hali. Ndipo wazee wa jadi wakasema kwamba *ngo samis muriat kobo kot nebo.*

b) *Makiesee chebo chepto*
   Tusitegemee vya mwanamke (msichana)

Paliishi familia moja katika kitongoji kimoja cha Kaptebeson ambayo ilijaliwa kupata wana tisa. Watoto wenyewe walikuwa wa kike, na ambao walilelewa kwa hali na mali. Wazazi wao waliwalea binti hao tisa kwa njia iliyokuwa ya kupigiwa mfano katika kijiji kizima. Binti wale kwa kujua kuwa hapakuwa na mwanamume yeyote, walitia bidii za mchwa kuhakikisha kwamba wavyele wao hawakukosa lolote. Shughuli zote za nyumbani sawa na shambani walizifanya kwa juhudi zao zote. Ghala lilijaa likatapika vyakula vya aina aina.

Zilipita miaka nyingi wazee wao wakaendelea kukonga. Kadri walivyokonga ndivyo mapengo yalivyoshuhudiwa ndani ya familia hiyo. Hii ilitokana na wanao kuolewa, jambo ambalo walililaani kimoyomoyo lakini wafanyaje? Ndio mpito wa maisha eti! Kitinda mimba alipoozwa, ilikuwa kama msumari wa mwisho ulipigiliwa kwenye jeneza la upweke na masaibu kwa wazee wale. Hapakuwa na yeyote wa kuwatafutia chakula, kutema kuni na hata kuwapikia. Waliishi tu kwa rehema za wahisani ambao walikuwa jirani zao, hisani ambazo hazikutegemeeka. Kila walipotupia jicho ghala lao, walilaani asasi ya ndoa, wakatamani wangalizaa angalau mwana mmoja wa kiume, kwa sasa angaliwafaa. Maisha yao yalizidi kudorora kila kulipokucha. Hazikupita miaka mingi kabla ya wao kuaga. Kijiji kizima kiliomboleza mauko ya wazee hao. Kila mtu akafungua jicho la ndani na kung'amua umuhimu wa mwana wa kiume katika familia. Kisa hiki kikawa chanzo cha msemo: "*cheptab ooreet age ne weendii ooreet age."* Hadi wa leo watoto wa kiume hudhaminiwa sana. Vie vile, Wahenga wa zama hizo hawakuchela kukitungia methali kisa hicho kama funzo kwa jamii kuwa '*Magiesee chebo chepto'* (Tusitegemee vya wanawake).

## Methali zilizotokana na Mazingira na Utamaduni

Kuna methali zinazohusu mazingira au utamaduni wa mahali fulani. Kwa mfano, wakaazi wa maeneo makavu, wana methali ambazo hueleza hali hiyo ya ukame. Watu waishio milimani, nao wana methali zinazohusu maisha ya milimani. Jamii ipatayo njaa mara kwa mara kwa ajili ya ukame wa eneo lao bila shaka wana methali zinazohusu njaa.

Kama tulivyotanguliza mwanzoni, jamii ya Wanandi wanaishi katika maeneo mbali mbali ya Bonde la ufa. Maeneo yao yanatofautiana kijiografia. Kwa mfano, Wapokot na baadhi ya Wamarakwet wanaishi katika maeneo kame. Wanandi na Wakipsigis wanaishi katika maeneo ambayo yana mito mingi na yenye rotuba. Kwa hivyo, tofauti zao za kimazingira na utamaduni zinaibua methali tofauti.

Tazama methali hizi:

a) *Magiumee saasuur ye moo-en keebet* (Tusiukate mmea wa *saasuurweet* masika yaishapo)

Mmea wa *saasuurweet* ni mmea unaofanana na mgomba (ndizi) ambao humea katika kingo za mito. Una majani mkubwa na mapana kuliko ya mgomba. Majani haya hutumiwa kama mwavuli kunaponyesha. Mmea huu hupatikana sana katika maeneo yenye mvua nyingi kama vile Nandi na Kericho. Kwa hivyo, Wakipsigis na Wanandi wanatumia methali hii kwa kuwa wanaufahamu mmea wenyewe. Watu wa maeneo mengine wakisikia methali hii huenda wakashangaa, kwa sababu ni mmea mpya kwao ambao hawaufahamu.

*b) Magiiboorchin pugener koima* (Usikoke moto karibu na *pukenereek*)

*Pugenereek* ni aina ya mimea ndogo ndogo inayofanana na uyoga. Mimea hii huchupua msimu wa mvua nyingi hasa juu ya vichuguu vya mchwa. Wenyeji wa maeneo kunapochipuka mimea hii huitumia kama kitoweo na kuliwa kwa sima. Kama ilivyo ni kwamba, huchipua katika mazingira yanayopokea mvua kiasi cha haja. Kwa hivyo, jamii kama vile ya Watugen, Wapokot na baadhi

ya Wamarakwet hawafahamu methali hii. Sababu ni kwamba, haipatikani katika maeneo yao. Ndiyo maana tulisema kuwa methali hizi zinahusu mazingira fulani tu, au utamaduni fulani.

## Uainishaji wa methali

Methali ni semi zenye busara zitoazo maadili mbalimbali katika maisha ya mwanadamu. Methali zinajulikana kama *Kaleweno-iik* ambazo katika jamii ya Wanandi zipo katika makundi manane, ambapo yameainishwa kwa mujibu wa matumizi yake katika jamii. Uanishaji huu unatokana na kile ambacho methali husika inasisitiza mathalan, undugu, ujamaa na kadhalika.

1. **Methali za Undugu (*Kaleweno-iik chebo biigaap ooreet ak tupchoosiek)***

Fungu hili ni la methali ambazo zinasisitiza undugu na utangamano wa watu katika zao moja. Hutumika kuleta utangamano miongoni mwa watu wenye uhusiano wa damu au ukoo mmoja. Kwa mfano;

*a) Ngo samis Muryaat kobo koot nebo* (Hata ikiwa panya yuavunda, ana kwao)

Maana ya methali hii ni kwamba hata kama mtu ni mbaya machoni mwa wanajamii, ana kwao, mahali ambapo anapokea mapenzi ya dhatikutoka kwa jamaa zake.Huwasuta watu wa aila moja kupendana kwa vyovyote vile.

b) *Ingen tariit koonnyii* (Kila ndege ajua kiota chake)

Methali hii inasisitiza umuhimu wa nyumbani kwa mtu na jamaa zake.

c) *Tuupcho weeriit ak kwaanda ko-uunotok chepto ak kaamet* (Baba na mwanawe wa kiume ni kama kaka wa zao moja kama ilivyo mama na mwanawe wa kike.)

Hapa msisitizo ni mapenzi ya dhati yanayotarajiwa kati ya wazazi na wanao. Ilivyo ni kwamba makuzi ya mwana wa kiume yanategemea maelekezi ya baba kama ilivyo kwa mama na mwana wa kike.

2. **Methali zinazohusu Maisha kwa jumla *(kaleweno-iik chebo sobeet komuguul)***

Kundi hili linahusu zile methali zinazotoa mwongozo wa maisha ya mwanadamu kwa jumla. Mifano;

a) *Ng'waan eng' kuut siise eng' moo* (Hata kitu kiwe chungu mdomoni, ifikapo tumboni hupoa)

Matumizi yake ni kutoa wasia dhidi ya malalamishi. Kwa mfano mtu apendaye kulalamikia chakula kwamba hakijaiva, si kitamu n.k huambiwa methali hii ili aepukane na tabia kama hizo na kuvumilia hali kama hizo.

*b) Ngobo kipng'ulya kobo, ngobo poisio kobo* (Kila kitu kina wakati wake)

*Kipng'ulya*ni mzaha. Kwa hivyo mtu apendaye mzaha sana hutahadharishwa dhidi ya maafa yanayoletwa na mzaha wake. Na hasa wakati masuala muhimu yanazungumziwa, hivyo kumwepusha kutoka katika hatari inayoweza kusababishwa na mzaha wake.

c) *Kisubee kipchaabeet kipchaabeet (*Mshale hufuatishwa mshale (Dawa ya moto ni moto))

Adhabu ipokezwe kulingana na makosa. Kwa mfano, mtu anapokosa apewe adhabu kulingana na kosa lake ili iwe funzo kwake na onyo kwa wengine wasidhubutu kufanya kosa kama hilo. Aidha, hutoa mwelekeo kwa wanaotoa adhabu ili wawe waangalifu wasije wakawa na mapendeleo.

**3. Methali zinazoangazia Ujamaa (*Kaleweno-iik chebo piigaab kookweet)***

Maisha ya ujamaa ni sisitizo kuu miongoni mwa jamii ya wakalenji. Ili kuishi kwa utangamano katika kijiji na hata wanajamii ambao ni jirani zao, kuna methali zilizobuniwa kuwaleta wanajamii pamoja na kuishi kwa utangamano. Mara nyingi methali hizi huelekezewa kwa wanajamii wanaotaka kujitenga na wanajamii wengine (wanaopotoka kimaadili/wanaokengeuka).Mifano ya methali kama hizi ni;

*a) Kergeey laagoi ak kiiyak* (Watoto ni kama mifugo)

Hapa watoto wanalinganishwa na mifugo kitabia, kwamba ni wepesi wa kusahau walichotahadharishwa. Kwa mfano, ng'ombe akiwa machungani hawezi kuingia katika shamba na kuharibu mimea ikiwa mchunga wake yuko, lakini pindi atokapo huingia. Hivi ndivyo walivyo watoto. Mara nyingi wanahitaji kuelekezwa kwa karibu sana. Pale pasipo mwelekezi, wao huwa waharibifu sana. Methali hii kwa hivyo, huambiwa mtu anayependa kulalamikia mienendo ya watoto wadogo. Hapa anakumbushwa kuwa wanahitaji jicho la karibu sana.

b) *Koonyit ko toroor, tee tany' ak muren* (Heshima ni muhimu kama alivyo ng'ombe na mwanaume)

Mwanaume na ng'ombe ni uti wa mgongo wa jamii ya Wanandi. Ili pawe na utangamano katika jamii, ni sharti heshima idumishwe kwa kuwa ndio msingi wa wa utangamano na fanaka katika jamii.

c) *Tangee-amei keya-ei* (Tunafaa kula jasho letu)

Watu wanaopenda kushirikiana na wenzao wakati wa raha au mapato mazuri bali hawataki kuhusika katika juhudi za kutafuta huambiwa methali ili kuwasuta kuacha tabia hiyo.

**4. Methali zinazosheheni Utu *(kaleweno-iik chebo chameetaapkeey)***

Methali hizi husisitiza utu wema katika jamii.

Mifano;

a) *Magibo-uunee gaa muguulel, kibo-uunee pu-oon* (Familia haiongozwi kwa moyo bali kwa mapafu)

Wanandi wanaamini kwamba ni vigumu kwa moyo kushawishika ikilinganishwa na mapafu. Kwa hivyo, katika methali hii, moyo na mapafu imetumika kijazanda kwa maana kwamba nyumba nyumba ikijengwa kwa moyo, ni vigumu kunawiri. Kwa hivyo, inafaa kujengwa kwa njia ambayo inaruhusu ubadilishanaji wa mawazo ambayo ni muhimu katika kuwatangamanisha wanajamii.

b) *Ngoriirchi laakwa rootwo kigoochin keet* (Mtoto akililia kisu mpe kijiti)

Unapogundua kwamba mtu amepotea au yuko katika hatari ya kupotea, jaribu kumwelekeza kutoka kwa ile hatari. Aidha, methali hutumika katika hali ambayo ni vigumu kuhusiana na mtu kwa njia isiyokwaza. Katika hali kama hii, methali hii inamhamasisha mtu kukumbuka kwamba mtu yule mwingine pia ni mwanadamu na hivyo, kwa lolote afanyalo afanye kwa utu.

c) *Weeksei uorwoon po keet* (Kivuli cha mti hurudi)

Watendee wenzako jinsi unavyotaka wakutendee. Methali hii huwafunza watu kuwatendea wenzao jinsi wanavyotarajia kutendewa. Kwa mfano, ukiwatendea wenzako mabaya, nawe usitarajie kutendewa wema.

d) *Magiroorechin soloomwo (*Usimcheke kilema)

**5. Methali zinazohusu hekima *(kaleweno-iik chebo ng'oomnoteet ak ng'ulotiet)***

Hekima ni jambo azizi katika maisha ya mwanadamu. Hukuzwa kila siku ya maisha ya mwanadamu mradi awe mwenye akili razini. Kwa hivyo, kuna methali zinazosisitiza hekima katika maisha ya mwanadamu.

Mifano;

a) *Kitestoo ng'oomnot ng'ulootyo* (Maarifa huongezwa hekima)

Ili mtu atekeleze mambo kwa urazini, anahitaji hekima kuongezea kwa ujuzi aliyo nayo.

b) *Magitestooy chebo tany' pei (*Maziwa na maji hayachanganywi)

Maziwa na maji imetumika kijazanda kwa maana ya ukweli na uongo. Hii ina maana kwamba ukweli na uongo uchanganywapo hutatanisha na hivyo watu hawawezi kupata suluhu kwa tatizo/matatizo yanayojiri.

c) *Kigilei kotkoimen* (Hekima hukuzwa kila uchao)

Hapana mwisho wa maarifa. Huendelezwa kila siku ya maisha ya mwanadamu. Kwa hivyo, akili razini ni ile iliyo tayari kupokea elimu na hekima wakati wowote.

*d) Agot ngo ing'oom komecherchiniigeey met* (Mwerevu hajinyoi)

Kijana muungwana, mtiifu lakini hatajiriki….anahitaji kuongezewa hekima ya kutekeleza maarifa yake.

6. **Methali zinazohusu Tahadhari *(kaleweno-iik chebo riibeetaapkeey)***

Hizi ni methali zinazolenga kuonya wanajamii dhidi ya mienendo potovu.

Mifano;

a) *Ng'oom chooriin kotamnee kiniindet* (Japo mwizi ni mwerevu, hamshindi mpelelezi)

Hata mwizi awe mjanja kiasi gani. Ipo siku atapatikana.

b) *Magibeeljiindoos kirogoon a-eeng'* (Fimbo mbili hazichomwi (hazitengenezwi) kwa wakati mmoja)

Ni tahadhari kwa watu ili kuepukana na shughuli nyingi kwa wakati mmoja. Huenda ukakosa kukamilisha hata moja.

c) *Magiteschin peek tereet agobo peek mustaay* (Usizidishe maji chunguni ikiwa posho ni wa kuazima)

Tusijitafutie shida nyingi wakati tumeshindwa kumudu kidogo tulizo nazo.

7. **Metahli za ubahili na ubinafsi *(kaleweno-iik chebo mo-eenateet)***

Ujamaa ni jambo ambalo hukuzwa katika jamii. Yeyote anayeishi maisha ya ubinafsi hutengwa. Kwa hivyo, kuna methali ambazo hutumiwa kuwasuta watu wanopenda ubinafsi na uchoyo.

Mifano;

a) *Ng'waan kobo chii tanduus(anyiny') kobo tyoony'* (Chungu kwa mwanadamu bali tamu kwa mnyama)

Mnyama ni neno ambalo limetumika kijazanda katika methali hii kwa maana ya 'mtu mwingine.' Hii ina maana kwamba mtu akipatwa na shida anahisi uchungu lakini yamsibupo mwenzake, yeye huwa hahisi lolote. Methali hii hutumiwa kuwatahadhirisha watu dhidi ya hali na hisia za wenzao. Huambiwa hasa wale wanaohisi uzito wapatwapo na shida, lakini shida iwafikapo wengine, wao hawajali.

b) *Kagereer seese kuut* (Mdomo wa mbwa umepasuka)

Methali hii hutumika kudhihaki walafi wasioona haya.

c) *Kibar moo kimageet* (Ulafi ulimuua fisi)

Fisi ni mnyama anayejulikana kwa ulafi. Kwa hiyo, methali hii hutumiwa kuonya watu dhidi ya uroho ambao una madhara makubwa kwa mwanadamu kiasi cha hata kusababisha kifo.

## 8. Methali zinazoonyesha majivuno na kiburi *(kalasunetaapkeey ak meenoteet)*

Majivuno na kiburi ni uovu ni tabia ambazo zinakemewa sana katika jamii. Ni kwa sababu hii ambapo methali zinazokashifu mienendo ya namna hii zilitungwa kwa ajili ya kukosoa hasa wenye nafasi katika jamii kama vile viongozi na matajiri.

Mifano;

a) *Makimenee metip talamwa* (Usijivunie kichwa cha nzige)

Matajiri wanafaa kuwa wanyenyekevu iwapo wanataka kuheshimiwa.

b) *Magiilasugeey amailaasuun kookweet* (Usijisifu, ngoja usifiwe)

Hii ni onyo dhidi ya ufidhuli au kiburi na ubinafsi. Hata kama umejaliwa, usijishauwe na kujitanua (usijisifu). Watu watakusifu tu pindi waonapofanaka kwako.

9. **Methali za kutia shime *(Kaleweno-iik che kicheersee)***

*Oo beelyoo amaiye saram* (Japo ndovu ni mkubwa hazai mapacha)

Methali hii ina maana kwamba hata mtu awe na uwezo mkubwa aje, juhudi zake hutegemea kudura ya mwenyezi Mungu. Ndipo wanafananisha ule ukubwa wa ndovu na uwezo wa kuzaa. Hutumiwa kuwatia moyo watu wanaoonekana kukata tamaa katika maisha. Kwa mfano, mtu anayefanya bidii na mwishowe hafanikiwi kama alivyotarajia. Kwa hivyo, huambiwa methali hii kwa lengo lakumkumbushwa kwamba ni muhimu kuridhika na kile kidogo alichokipata. Methali hii inaweza kulinganishwa na methali ya Kiswahili isemayo, heri nusu shari kuliko shari kamili.

## 5.0 Hitimisho

Kutokana na yaliyoangaziwa katika makala haya, tunaweza kusema kuwa methali si misemo tu inayotumiwa kueleza jambo kwa njia ya taswira na kwa ufupi ili kutoa maadili au onyo. Jambo muhimu ni kutambua kwamba methali ni sanaa ya maneno yenye hekima, na yanayosanifu amali za jamii inayohusika kwa kuzingatia kwa mfano mazingira na utamaduni wa jamii husika. Aidha, ni wazi kwamba kila uwanja wa maisha ni chemichemi ya kuundia methali. Kwa hivyo, ipo haja ya kufahamu kwa undani mazingira na utamaduni wa jamii, na kila panapotokea mabadiliko makubwa katika uwanja muhimu wa maisha, basina methali ziundwe kutokana na mabadiliko hayo. Huenda busara ikabaki ile ile lakini namna ya kuieleza itabadilika kutegemea mabadiliko ya mazingira.

**Marejeleo**

Finnegan, R. (2012). *Oral Literature in Africa.* Cambridge. Open Book Publishers CIC Limited.

Lubaleje, Y. (1990). Methali Zetu: Maudhui, Lugha na Muundo. Katika *Jarida la Kiswahili*. JK. Na.2. Dar es Salaam: Standard Publishing Company.

Momanyi, C. (2006). Dhima na Utendakazi wa Vitendawili katika Jamii. Katika: C. Njogu, C. Momanyi, & M. Mathooko (Whr.) *Fasihi Simulizi ya Kiswahili*. Nairobi: Twaweza Communications. Uk. 19-28.

Mulokozi, M.M. (1989). Tanzu za Fasihi Simulizi; katika *Mulika*: Na. 21. Dar es Salaam: TUKI

RoK (1999). Population Census. (Statistical Abstract 2010 Central Bureau of Statistics, Nairobi: Ministry of Planning and National Development).

Saidi, M.V. (2006). "Fasihi Simulizi na Utamaduni: Utamaduni, Maana na Matumizi ya Methali za Kidigo." Katika: Njogu, C., Momanyi, C. na Mathooko, M (Whr.) *Fasihi Simulizi ya Kiswahili*. Nairobi: Twaweza Communications. Uk. 19-28.

http://www.ethnologue.com/language) 9/08/2015. 11:33 am